

# Building Deeper Relationships

using Faith-Based Facilitation

# Building Deeper Relationships

## using Faith-Based Facilitation



Makala haya yalichapishwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 2010 na makao makuu ya kitaifa ya Jeshi la Wokovu, London/Haki za uchapishaji @ 2010 Makala yote pamoja na maneno, sanaa na michoro yote imetegemea wakfu wa Jeshi la wokovu.

Marejeleo yote ya Biblia yametolewa kwa Biblia ya New Revised Standard Version isipokuwa pale ambapo tafsiri nyingine imeonyeshwa kwa alama za mabano.

Maelezo kuhusu uchunguzi wa visa maalum: Mifano yote katika makala haya imetolewa kutokana na mifano ya maadili mema ya vipindi vya Jeshi La Wokovu isipokuwa majina, mahali na mambo mengine yamebadilishwa, kukubalika na kuambatanishwa.

Makala haya yametayarishwa kwa usaidizi wa pamoja wa Jeshi la Wokovu,NORAD naTEARFUND.Yametolewa na Makao Makuu ya Kimataifa yakishirikiana na Oxford Centre for Ecclesiology and Practical Theology.Judith Thompson,mwanatheologia,mwalimu na mwandishi, alichangia katika makala ya awali.Makala hayo yalirudiwa,yakahaririwa kisha makala mapya yakatayarishwa na Waumini wa Jeshi La Wokovu walio na ujuzi mkubwa ulimwenguni kote na ambao hutumia mafundisho ya kidini kufunza wanajeshi,kanisani,vituo,maendeleo ya jamii,huduma ya afya,wilaya,mikoa na hata makao makuu ya Kimataifa.

## Utangulizi

Mufunzo kuhusu namna ya kujenga uhusiano mwafaka ni jambo muhimu kwa kila mtu.
Mara nyingi uhusiano hupingwa na unaweza kuathirika pakubwa.
Wakati mwingine huvunjika.Uhusiano wa familia, marafiki, majirani, wenzako unaweza kuwa mzuri.Uhusiano unaweza kuwa wa maana zaidi kila wakati
Mafundisho ya Kidini ni njia ya kusaidia watu kufikiri, kuzungumza na kutafakari na kisha kujaribu kusuluhisha mambo hayo kupitia kwa imani.Matokeo yake ni watu walio na afya nzuri na jamii iliyonawiri katika mahusiano mwafaka.Mafundisho ya Imani si itikadi wala mradi-ni njia ya utendaji kazi.Siyo jambo jipya lakini linahitaji kufanyiwa mazoezi, kukumbukwa na kutekelezwa.Linahitaji kuwa mazoea.
Kuipa hali hii jina na kuihusisha na vifaa/mbinu mbalimbali pamoja na elimu ya kidini litakuwa jambo jipya kwa watu wengine.Mafundisho ya Imani yatakusaidia kuwa na mtazamo mpana wa mambo na matukio ya kila siku kwa upana na kutafuta njia za kuyashughulikia kupitia kwa imani.Watu wanaweza kuelimishwa kuhusu mbinu za kuhusiana kisha wafuzu kuwa waalimu wa Mafundisho ya Imani.Hivyo wanaweza kuwa na makundi (au kutumia mbinu hizo katika mahusiano yao ya kila siku) kuboresha uhusiano katika jamii zao.Mtazamo huo si tofauti na mambo ya kawaida ya  Jeshi La Wokovu lakini yanafaa kushirikishwa katika misingi ya uongozi na utendaji kazi.

### Tunafanya nini na kwa nini tunakifanya?

Mbinu za uwasilishaji zimefundishwa katika Jeshi La Wokovu kwa miaka mingi.Aliyekuwa kiongzi wa Kimataifa wa Jeshi La Wokovu, Generali Mstaafu, John Gowans, alisisitiza umuhimu wa Uwasilishaji Wa Kiimani aliposema:'Ni lazima tuendelee kurekebisha tunachokifanya na sababu za kukifanya.'

Mpangilio unaotumika katika Uwasilishaji wa Kimani unafanana na njia zingine za kufanya kazi kama vile utaratibu wa elimu,utaratibu wa mipangilio wa biashara na utaratibu wa usimamizi wa miradi.Hili lisiwe jambo la kushangaza-watu hutumia njia nzuri wanapofundishwa,kufanya biashara au kutekeleza mradi.Kijitabu hiki kinaonyesha namna watu wa imani wanavyoweza kutumia utaratibu  huo ambao unashirikisha maoni kutoka kwa Imani ya Kikristo.Ingawa mtindo wa UWK ni mpya kwa wengine,kuna uwezekano kuwa wametumia pasipokujua mtindo kama huo wanapokabiliwa na hali ngumu.

> **Zingatia:** Ni muhimu kwa wawasilishi wa kiimani kutambua, utajiri mwingi, vipawa na uwezo wa wa kila mtu, familia zao, marafiki na jamii zao.Hata yule masikini hohe hahe ana kipawa cha kipekee na uwezo ambao unahitaji kutambuliwa na kukubalika..

### Umuhimu wa imani

Kwa miaka michache iliyopita, kumekuwa na hali ya kutaka kujua tofauti zinazoletwa na imani katika kuboresha maisha ya wanajamii.Wajuzi wengi walitarajia athari za imani duniani kushuka katika miaka michache iliyopita.Mawazo yao yamedhibitishwa kuwa uwongo.Dini in nguvu ya ajabu katika dunia ya kisasa na uwezo wake unaendelea kukuwa.Kwa hivyo mashirika ya kidini yamekuwa yakiulizwa kueleza namna imani inavyochangia katika utendaji kazi.Uwasilishaji wa kiimani unaweza kusaidia kujibu maswali haya. Uwasilishaji wa Kiimani unasaidia kuonyesha sababu za kuchukua hatua, matokeo ya hatua zilizochukuliwa na husaidia kutambua matokeo kwa jumla.
Ingawa uwasilishaji hutumiwa na mashirika yasiyo ya kidini,haihitaji kuwa njia ya pekee ya kufanyia mambo ulimwenguni.Kama vile muziki unavyopendwa sana na watu wa ulimwengu,lakini pia ni sehemu katika ibada za kikristo,ndiyo uwasilisaji huweza kuchukua nafasi muhimu katika kazi yetu.Vile makala haya yanavyoelezea,Uwasilishaji wa imani unaweza kulinganiswa  na jinsi Roho Mtakatifu alivyo , 'Njia ya kumfikia

Mungu' hutumika ulimwenguni.Uwasilishaji wa kiimani husaidia watu 'kufikiana' mmoja na mwingine-hukuza uhusiano,husaidia watu kujali wengine na hubadilisha ulimwengu unaopendwa na Mungu. Uwasilishaji wa Kiimani husaidia watu kushirikisha imani na matendo yao.Watu walio na imani kwa Mungu hutaka kumhusisha Mungu kwa kila jambo katika maisha yao.Wale wa imani tofauti wana msukumo uo huo unaotokana na msingi wao wa imani. Kijitabu hiki kimeandikwa kwa mtazamo wa kikristo kwa sababu Jeshi La Wokovu ni Kanisa la Kikristo
Hata hivyo, watu wasiokuwa na imani yoyote ya kidini bado waamini na kutenda mambo kutokana na msukumo wa imani na maadili yao.Mpangilio na mbinu zitumikazo katika Uwasilishaji wa kiimani zinaweza kusomeka na kutumika na yeyote-mradi tu waweze kusikilizana na kufanya kazi pamoja ili kuimarisha jamii.Jambo hili linaweza kuwapa nguvu na kuwafanya bora zaidi-hasa katika nyakati ngumu.Unaweza kutumika unapotangamana: na watu;katika kundi la aina yoyote; Kwa t+erritori;mkutano wa kitaifa au kimataifa.




## Mfano wa Uwasilishaji bora wa kiimani

Maafisa wa Jeshi La Wokovu, Majemedari Ruth na Andrew, waliooana, walichukua wadhifa mpya wa cheo cha maafisa wa kikao Walikuwa wamepata mafunzo ya mbinu za uwasilishaji, hasa katika usikilizaji mwema, halafu wakapanga mkutano na maafisa wengine ili kupanga mikakati ya namna watakavyoendelea mbele.
Watu walifurahia walipoulizwa maoni yao na mapendekezo mengi yalitolewa.Meja Andrew, ambaye alichukua nafasi ya mwasilishaji wa muda,aliorodhesha maoni yote.Kisha akawauliza njia bora ya kupata mambo yanayoathiri jamii zao.Washiriki katika makundi waliamua kutembelea angalau familia 50 ambazo hazikuhudhuria mkutano.Meja Andrew aliwapa wageni hawa mafundisho ya kimsingi akawakumbusha wasitoe majibu kwa maswala yaliyoibuka na pia wasiahidi chochote.Walihitajika tu kusikiliza,kutazama,na kuahidi kurudi kuwatembelea wakati mwingine.

Baada ya mkutano wa kwanza,walikutana na kila mmoja akasema alichokuwa amegundua.Baadhi ya wailokuwa wametembelewa walialikwa ili kuelezea maoni yao.Meja Ruth ndiye alikuwa mwasilishaji.Alihimiza kila mmoja wao kuzungumzia kila alilokuwa ameona au kuambiwa.Baada ya muda mfupi walikuwa na orodha ndefu,lakini mfululizo wa mambo mazuri mahitaji ulianza kuonekana.Jamii hii ilikuwa imebarikiwa na kuwa na wazee wengi na hata kina mama na watoto wachanga.Wengi katika makundi haya mara nyingi pia waliishi nyumbani kwao na ilisemekana na watu tofauti kuwa waliona upweke.Wauguzi wengi waliostaafu na waalimu pia waliishi na familia zao karibu nao.Wengi waliotembelewa walisema hawakujua la kufanya na muda waliokuwa nao.
Meja Ruth aliuliza kundi hilo:'Tunawezaje kusuluhisha matatizo haya?'Tena yeye kama mwasilishaji aliwahimiza kutoa mapendekezo yao. Watu tofauti walitoa maoni tofauti kama:

- Mikutano ya wazee ambapo wanaweza kuelezana visa vyao
- Vipindi vya masomo ya Bilia kwa akina mama walio na watoto wachanga
- Elimu ya kimsingi kuhusu mambo ya afya kwa makundi yote ikiongozwa na waalimu waliostaafu
- Miradi ya kuzalisha pesa ili kuwasaidia walio na mapato ya chini kugharamia afya yao

•Mikusanyiko ya wana-jamii ambapo watu wanakula na kuimba pamoja
•Kutembelea jamii zingine

Mojawapo wa mshiriki mgeni wa kikao, Mary, alidokeza kuwa takriban shughuli hizi zote zilijumuisha wanajamii kuimarisha ushirikiano.'Kwa nini tunatarajia waje kwetu?' aliuliza .Kwa pamoja walijadili kile wangefanya.Meja Andrew aliangazia kwa ufupi jinsi Yesu alifunza na kuponya alipokuwa ulimwenguni.Meja Andrew alielezea umuhimu wa wakristo kuwafikia watu katika jamii zao
Baada ya mjadala wa kusisimua,kundi hili liliafikiana kujaribu mambo matatu:
1. Mary alikubali kupanga matembezi ya mara kwa mara katika jamii ili kukutana na watu, kutafuta marafiki na kujadili mambo yanayotatiza.Alikaribisha kila mtu kushiriki matembezi-washiriki wa Jeshi La Wokovu na wasiokuwa washiriki wao.

2 .Mkutano wa kila wiki katika ukumbi wa Jeshi la Wokovu ambapo watu wa zaidi ya miaka 60 wangealikwa.Kungekuwa na majadiliano kuhusu mambo ya kiafya huku wakinywa chai ya majani ya kienyeji,kusoma kifungu cha Biblia kisha kuimba na kuzungumzia maisha yao pamoja

3. Mkutano wa kila wiki wa akina mama wa watoto wachanga katika ukumbi wa Jeshi utakaolenga mambo ya kiafya, ukiwashirikisha wauguzi waliostaafu wanaofanyia zahanati za serikali zilizoko karibu.Wangefuatilia ukuaji wa watoto wakitumia vipimo na michoro ya kuagiza kutoka kwenye zahanati.Watoto wagonjwa wangepangiwa matibabu ilivyotakikana.Vilevile, la muhimu, kungekuwa na wakati wa akina mama kuimba, kuomba na kuwa na ushirika pamoja.
Kabla ya mkutano kufungwa kwa maombi,Jemedari Ruth na Andrew walihakikisha watu wamepewa majukumu mbali mbali.Tarehe zilipangwa na wote waliofanya matembezi ya awali waliahidi kutembelea tena waliokuwa wamewaona mbeleni.Wangewahimiza wazee na mama wachanga kuhudhuria matukio mapya na kuwaleta marafiki zao

Baada ya muda mfupi makundi yaliundwa na yakapendwa na kila mtu aliyehusika.Matembezi katika jamii yalifanya watu kuwaalika kuwatembelea nyumbani.Washiriki wa kikao walishangazwa na kiwango cha mafunzo waliopata kutokana na mazungumzo haya yanayohusu ujengaji wa uhusiano mwafaka.Sasa waliweza kuona mambo yaliyowapita mwanzoni.Kwa vile watu walikuwa wameshirikishwa,kila mtu aliona umuhimu wa kuchukua jukumu la mpango huo.Kwa kiwango fulani,mambo haya mapya yalianza kunufaisha maisha ya jamii nzima
Jemedari Ruth na Andrew walikuwa makini kufuatilia na kutathmini kazi ya makundi matatu makuu.Walikuwa na mikutano ya mara kwa mara na viongozi na washiriki wa makundi wakitafakari waliyokuwa wakifanya, wakirejelea utaratibu uliokubalika na wakfu wa Uwasilishaji wa Kiimani (rejelea sura ya 1 kwa maelezo zaidi) na maswali ya kujitathmini (rejelea sura ya 2).Haya yalisaidia ukuaji wa makundi, kunawiri na kukubali mabadiko yanayojiri katika jamii.
Uwasilishaji wa kiimani kama ulivyoonyeshwa na Jemedari Ruth na Andrew, umekuwa ukiendelea kila wakati watu wanapofanya kazi pamoja na kujenga uhusiano mwafaka.Viongozi waaminifu na walioimarika husikiliza, hushirikisha na kuhimiza washiriki wanapotafuta njia za kukabiliana na changamoto na hata nafasi wanazopata.



Uchunguzi unaohusu zaidi ya visa kumi unaoonyesha vile Uwasilishaji wa Kiimani umetumika katika hali halisi na unaweza kupatikana kwa from **www.salvationarmy.org/fbf.**




## Sura 1:
# Mpangilio wa Uwasilishaji wa Kiimani

Uwasilishaji wa kiimani ni mpangilio unaotumia mbinu maalum ili kusaidia watu kuwa na uhusiano mwafaka.UWK unategemea msingi ya uchungaji ambayo hutumiwa kusaidia watu wa imani katika kazi yao.Sura hii inaangazia mpangilio wa UWK na kupendekeza namna ya kusaidia watu kupitia kwa mbinu ya hatua tano.Sura ya 2 inaangazia mbinu hizo.

Ni muhimu kusisitiza kuwa UWK unahitaji utathmini wa kila wakati.Haukamiliki kwa (hatua ya 5), lakini kama mipangilio mingine, hufanyika mara kwa mara-kwa mzunguko/mviringo. 'Hatua' itakayochukuliwa katika jambo jipya ndio linakuwa jambo la kuchunguzwa na kutathminiwa katika raundi inayofuata ya UWK n.k

**Hatua ya 1:Shughuli/Jambo**

Mpangilio wa UWK huanza watu wanapotambua jambo linalohitaji mageuzi.Huenda likawa jambo muhimu au shughuli ya kawaida inayohitaji kuangaziwa zaidi ili kujua 'tunachofanya na sababu za kukifanya.'Kwa lolote lile, jambo hilo linahitaji kutambuliwa-hasa na kundi la watu wanaofanya mambo pamoja.

**Njia za kutekeleza Hatua ya 1**

LUjuzi wa kusikiliza ni muhimu kwa kila hali ya UWK (Mbinu ya 2.1).Matembezi ya nyumbani na utambuzi wa jamii imekuwa njia mwafaka ya makundi ya Jeshi La Wokovu kuelewa na kuthamini mambo mbali mbali katika jamii (Mbinu 2.3 na 2.4).

**Zingatia:** Makundi ya wawasilishaji ya Jeshi La Wokovu wamejifunza mambo manne ya kukumbukwa unapotembelea familia/jamii-Himiza,Tambua,Jifunze na Ufunze(HTJF).Yaani himiza watu kuongea(Himiza),Sikiliza maoni na kuzingatia mtazamo wao(Tambua),Jifunze kutokana na tajriba,hali na fikira zao(Jifunze),Chukua mafunzo yao kisha ufundishe watu wa jamii tofauti(Fundisha).

### Hatua ya 2: Eleza/Chunguza

Jambo/Shughuli iliyotambuliwa inaelezwa na kuchunguzwa kwa undani kabisa.Wanoayatafakari (mmoja mmoja au kwa kundi) hujaribu kufikikiria mambo yote yanayochangia kuwepo kwa jambo hilo.Haya hufanya mtu/watu kuelewa kwa undani hali hiyo.Jambo lolote linalokabili jamii lisielezwe tu kijuujuu.Kuwa na mtazamo pana iwezekanavyo. Hakikisha umezingatia tu maelezo na uchunguzi na usitoe hukumu wala maoni.

#### Mbinu za kutekeleza Hatua ya 2

Tambua uzuri na uwezo wa mtu(Mbinu 2.6).Jambo litakalomsaidia mwasilishaji wa kiimani ni utajiri, vipawa,na uwezo wa watu ,familia na marafiki zao,na jamii zao.Hata Yule masikini kabisa ana vipawa na uwezo umbao unafaa kukubaliwa na kutambuliwa.
Majadiliano(2.5) husaidia kupata maelezo mwafaka kuhusu jambo linalotendeka
Kutambua mipaka ya jamii (Mbinu 2.5) ni mbinu muhimu kutumia unapotembelea jamii mara ya pili ili kupata ujumbe zaidi.

### Hatua ya 3:Tafakari/Chunguza

Hatua hii inahusu kutafakari mambo ambayo yametokea, kisha kuelezea mambo hayo na majibu yaliyotolewa.Watu wenye imani hupendelea maombi, kusoma maandiko na kuwaza kama mambo muhimu kati ya hatua ya 2 na 3.Uchunguzi unafanywa kwa makini katika hatua hii na maswali magumu yanafaa kuulizwa na kujibiwa.Kwa mfano, Je mradi huu bado unazingatia malengo yake ya awali? Hali hii inahusiana vipi na mafunzo ya Biblia.Ni mabadiliko yapi yanahitajika ili kuboresha zaidi maisha ya wote wanaohusika?
'Hali ya Kairos'inaweza kuonekana wakati huu wa kutafakari na kuchunguza (Rej.maelezo hapo chini).Matokeo hayo hayawezi kutabiriwa au kushurutishwa, lakini huenda yasitokee iwapo washiriki hawana mtazamo wazi.Zaidi ya maombi na kutafakari, matembezi, au 'kufikira kwa ubunifu' (Taz.Mbinu 2.6) huenda kukafurahisha watu zaidi. Uchunguzi na Kutafakari usiharakishwe wala kupuuzwa! Muda mwingi wa kutekeleza mpango wa UWK unafaa kutumia kwa hatua hii.

#### Mbinu za kutekeleza Hatua ya 3

Kuelezea(Mbinu 2.2)
Ubunifu wa kufikiri (Mbinu 2.9)
Mbinu ya kujitathmini (2.11) imependekezwa kwa kila kundi kutumiwa mara kwa mara



### Hatua ya 4:Amua/Fanya mipango

Muda uliotumiwa vizuri kuwasilisha hatua ya kutafakari kutumia UWK husaidia washiriki kufanya maamuzi ambayo wanayaajibikia na hata kuyatekeleza.Vikundi au watu binafsi wanaweza kuorodhesha uzuri na ubaya wa kila pendekezo.IIwapo kutakuwa na ugumu wa kuafikiana, itakuwa bora kuandika mambo yote ya kuzingatia ili kutekeleza jambo hili.Mambo haya yanapojadiliwa kwa kundi huenda wakaanza kuafikiana. Huenda ikawa vigumu kufikia uamuzi wa kukubalika na kundi lote ili kutekeleza jambo.Haya yakitokea,itabidi mwasilishaji aulize kundi kukubali uamuzi wa wengi huku akijaribu kuwashawishi walio na msimamo tofauti

#### Ili kuhakikisha kuwa mambo yaliyopendekezwa

yametekelezwa,itakuwa vizuri kuuliza:
Ni vifaa/mbinu gani zilizopo ili kufanikisha mpango huu? Mapengo yatazibwa vipi?
Nani atasimamia kila mpango uliopangwa na utatekelezwa lini?
Mafunzo yapi na/au usaidizi upi utatakikana?
Tahadhari zipi zitazingatiwa?
Matatizo yatakabiliwa vipi?
Nani anastahili kujulishwa mipango na atajulishwa na nani?
Matokeo yatahaririwa lini?

**Mbinu zilizopendekezwa:**

Kutambua uzuri na vifaa (Mbinu 2.6) ni mbinu muhimu kutumia katika hatua hii ili kuhakikisha kuwa itawezekana kutekeleza maafikiano
Kuipa (mbinu 2.6) kipau mbele itasaidia kufanya uamuzi kutokana na mapendekezo tofauti.



**Zingatia:** Iwapo vifaa vitahitajika kutoka kwa territory/komandi,Mtindo wa CPMS unafaa kutumiwa kutayarisha mwongozo

### Hatua ya 5:Utekelezaji

Ni muhimu kutekeleza maamuzi.Kumbuka kuorodhesha vipengele vya utekelezaji,chunguza athari za utekelezaji kisha ukusanye ujumbe unaofaa.Haya yatahitajika katika sehemu inayofuatia kwenye hatua ya 2 na 3 na inaendelea.Mpangilio wa UWK haukomi katika hatua ya mwisho,lakini unaendelea hivyo.Baada ya Hatua ya 5 Utekelezaji,mabadilliko yaliyofanywa yataendelea kwa hatua mpya:

**Hatua mpya ya 1** Shughuli/Jambo

Hatua inayochukuliwa kutokana na hali hii italeta mabadiliko na hivyo kutakuwa na 'hisia tofauti ' katika hatua ya 1

**Hatia mpya ya 2** Eleza/Chunguza

Maelezo mapya na uchunguzi wa hali iliyobadilika yatahitajika (Ni muhimu kufanya jambo hili kwa uangalifu.) Unaweza kushangazwa na kiwango cha mabadiliko yaliyosababishwa na hatua iliyochukuliwa.

**Hatua mpya ya 3** Tafakari/Chunguza

Hii ni sehemu muhimu ambapo mabadiliko yaliyoletwa na hatua iliyochukuliwa yanaweza kutafakariwa na kuchunguzwa.Ni muhimu kufanya hivi kabla ya kuendelea na hatua ingine.Huenda ikasaidia kupumzika kidogo wakati huu, ili kujua athari za hatua iliyochukuliwa zitakavyokuwa muda mrefu baadaye.

## Kuweka imani

Uwasilishaji Wa Kiimani hutambua mambo matatu muhimu kama nguzo ya mwongozo katika Jeshi La Wokovu:

1.Biblia
2.Desturi za Kanisa
3.Uhimizo wa Mungu kulingana na hali ya Kairos

## Biblia na Desturi ya Imani

Watu wa imani huongozwa na mafundisho yanayopatikana kwa kizazi kimoja hadi kingine. Jeshi La Wokovu,likiwa kanisa la kikristo linaamini kuwa maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya yaliandikwa kulingana na himizo kutoka kwa Mungu,na ni mwongozo muhimu utokao kwa Mungu ambao husaidia watu kuishi maisha ya maana zaidi

Kanisa la Jeshi La Wokovu halitoi mamlaka sawa kwa desturi za kanisa kama Biblia.Hata hivyo,tunatambua kuwa kuna mengi ya kujifunza kutokana na maisha na mafundisho ya Wakristo ambao wametangulia mbele,hivyo basi mafunzo yaliopatikana na mwongozo ulioachwa na desturi ya imani unafaa kuchunguzwa na kutafakariwa kwa maana utaleta mawazo muhimu mara kwa mara

**Zingatia:** Wawasilishaji wa Uwasilishaji Wa Kiimani wanahitaji kutadhari athari zinazoweza kuletwa na pesa katika hali hii-hasa pesa zinazoletwa kutoka nje ya jamii.Fedha za kutoka nje wakati mwingine zitahitatajika 'koungezea' zile zilizoko lakini kuwe na tahadhari ili hali hii isiongozwe na matakwa ya wafadhili.Inapendekezwa kwa dhati kuwa jamii izoee kutumia UWK kabla ya kuungana na wafadhili wa nje. Kwa njia hii watu katika jamii watagundua uwezo na vipawa vyao hivyo kuwa na ujasiri wanapoungana na wafadhili wa nje

## 'Hali ya Kairos'

Mawazo yanaweza kupatikana kwa dharura yanaweza kupatikana katika hatua yoyote ya mpangilio wa UWK lakini hasa wakati wa kutafakari/uchunguzi na maamuzi. Watu wa imani wanaweza kuhisi uwepo wa Mungu nyakati hizi.'Hali ya Kairos' ni neno.

linalotumiwa kuelezea hali hizi. Kuna kisa kinachojulikana sana cha




hali ya Kairos katika historia ya Jeshi La Wokovu.William Booth, mwanzilishi wa Jeshi La Wokovu, alimwambia mkewe, Catherine, aliporudi nyumbani baada ya mkutano katika East End ya London:'Mpenzi, nimepata kile nimekuwa nikitafuta maishani mwangu.'Alihisi Mungu akimwongoza katika njia fulani.William Booth alikuwa amehisi' Hali ya Kairos'.

Hapo mwanzoni Biblia imesema kuwa Petero ambaye alikuwa na Yesu kwa miaka miwili hatimaye alitambua Yesu ni nani kisha akasema: 'Wewe ni Kristo Mwana wa Mungu aishiye.'(Mathayo 16:16 NIV).Yesu alitoa hadithi za watu kuwa na mawazo yasiyotarajiwa kama vile mwana mpotevu( Luka 15:11-32) ambapo' akili zilimrudia (KV17)'huyo kijana baada ya kupitia matukio mabaya kisha muda mrefu wa kutafakari.Ni hali ya Kairos iliyomwunganisha na babake kwa shangwe.

Kairos ni neno la Kigiriki ambalo si rahisi kutafsiri kwa lugha zingine-linamaanisha kitu kama 'wakati wa Mungu' au 'wakati unaofaa.'Hisia hizo zaweza kutujia wakati ambapo hatumtafuti Mungu sana.Mawazo mapya yanaweza kutujia polepole lakini si kwa 'wakati 'maalum.UWK unayachukulia matukio haya kuwa kazi ya Mungu' Wakristo huamini kuwa Biblia, maombi na wakati wa kuwaza kuwa unaweza kusababisha hali ya Kairos.Hali ya Kairos imewekwe katikati ya picha kuonyesha uwepo na utendaji kazi wa Mungu kwa mambo yote maishani. Inawakumbusha watu wa imani umuhimu wa kuambatanisha imani na vitendo na ahadi kuwa Mungu yupo kila wakati.

### Sura ya 2:

## Mbinu za Uwasilishaji Wa Kiimani

Mbinu zilizoelezwa katika sura hii husaidia kutambua, kuidhinisha na kuhimiza matumizi ya vipawa na utajiri tulio nao. Mbinu hizi hazitatumika kila wakati. Ubora wa mwasilishaji mwenye mazoea unatokana na ule uwezo wa kuchagua mbinu inayofaa kwa wakati unaofaa katika hatua tano (inavyoelezwa kwenye sura ya 1).Haya hayawezi kupatikana darasani! Unahitaji kufanya mazoezi ya kuwa mwasilishaji wa Kiimani.

Huenda ukawa na mbinu hizi tayari-labda hata bila kutambua.Zingine zinaweza kufunzwa, kufanyiwa mazoezi na kukuzwa.Hakuna masharti kuhusu mbinu zipi zitatumiwa wakati upi.Mwasilishaji hodari anatakiwa kuwa na uzoefu wa mbinu zote zitumiwazo na UWK ili kuweza kuchagua mbinu mwafaka kwa kila hali. Orodha ifuatayo haijumuishi mbinu zote.Zingine zinaweza kutambuliwa iwapo zitasaidia watu kufanya mambo kupitia kwa mpango wa UWK.

### 2.1 Kusikiliza

Usikilizaji mzuri unahitajika kwa kazi zote za Uwasilishaji Wa Kiimani,na hutumika katika kila hatua ya mpangilio wa UWK.Watu wanaposikilizwa vizuri huhisi wamekubalika na kuthaminiwa na huwadhibitishia kuwa

wana umuhimu.Hizi ni baadhi ya zawadi nzuri tunayoweza kumpa mtu,hasa kwa yule aliyepoteza tumaini.Hata tunapokuwa hatuwezi kuwapa kitu cha kuwasaidia maishani, kipawa chetu cha kusikiliza kwa makini kinaweza kupunguza maumivu na shida.

Vile vile,usikilizaji mzuri hutuzuia kufanya makosa.Tunaposikiliza kwa umakini,huwa tunakadiria matatizo kwa undani na hiyo kuwa na nafasi nzuri ya kuwasaidia wanaotafuta njia ya kuendelea mbele,badala ya kusikiliza tu hivi hivi kwa sababu ya kutaka kusaidia kwa kutumia mawazo au mtazamo wetu.

Vibaya zaidi, tunaweza kujikuta kutoa suluhisho hata kabla ya kuelewa tatizo.Mbinu za usikilizaji mzuri zinaweza kusaidia lakini kivyake, hazitoshi.Usikilizaji mzuri huanzia moyoni.

**Usikilizaji mzuri ni:**

Kumsikiliza mwasilishaji kwa makini, ambalo ni jambo rahisi kusema kuliko kufanya, hasa kunapokuwa na watu wengi wa kusikilizwa ilihali muda hautoshi.Pia ni vigumu katika mazingira ya kelele ama tunaposumbuliwa na mambo mengine yanayotuzingira.Licha ya matatizo hayo, tunahitaji kulipa jambo hili kipau mbele.

Kuonyesha usikilizaji kwa mkao wa mwili, na ishara za hapa na pale au sauti za kuhimiza.Mheshimu mzungumzaji-usimkatize.

Kurudia kilichosemwa na mzungumzaji, ukianza na maneno kama'Sasa vile unavyoona...' ama 'Je ninaweza kuhakikisha kuwa nimeelewa unachosema?'





Kuyarudia  yaliyosemwa na msemaji kwa maneno yako, ukianza na vifungu kama,’Ninafikiri unachosema ni...’ama ‘Inaonekana kuwa...’Matumizi mazuri ya marudio mara nyingi husaidia mzungumzaji kutafuta maelezo zaidi bila kuuliza maswali. (Hayawekani! Ikiwa huamini, jaribu.) Wewe,kama msikilizaji,unapouliza maswali,hakikisha yamenuiwa kumsaidia mzungumzaji kufafanua au kuelezea zaidi anachojaribu kusema.Jihadhari usiulize maswali yanayowaelekeza kusema unachotaka kusikia (Taz.mbinu ya 2, Ufafanuzi)

Kutambua hisia za mzungumzaji kuhusu kile anachozungumzia.Hata hivyo tuhakikishe tumetambua hisia zake na kuzijua,lakini si kuonysha kile ambacho tungehisi tungekuwa katika hali yake

Kufupisha: Mzungumzaji akimaliza, jaribu kufupisha alichosema.Hii husaidia mzungumzaji kujua amesikilizwa, na husaidia mwasilishaji kujua walielewa kilichozungumziwa.Ufupisho ni muhimu kabla ya kuendelea na mbinu inayofuatia, Kufafanua Maswali.

**Zingatia:** Mwasilishaji bora ni yule anayezungumza machache,kazi ikisha tekelezwa lengo kufikiwa, watasema, ’Tuliyatekeleza sisi wenyewe’.(Lau Tzu,500 BC)

## 2.2 Kufafanua Maswali

Kufafanua maswali ni muhimu hasa katika Hatua ya 2 (Chunguza) na Hatua ya 2 (Kutafakari) mtindo wa UWK unapotumiwa

Kufafanua jambo na mtu au kundi huendelea vizuri kufuatia usikilizaji mzuri.Kila anayetaka kuzungumza akisha pewa nafasi ya kufanya hivyo,mwasilizaji anatakiwa kuuliza maswali kwa umakini kusaidia watu kutafakari waliyosema.Maswali yahusishwe hasa kwa mambo yaliyoshughulikiwa,lakini yanaweza kuanza kama mifano ifuatayo:
Sikufuatilia hasa uhusiano ulioko kati ya ulichosema kuhusu** na**.Unaweza kueleza zaidi kuhusu jambo hili?
Sikuelewa hasa ulichokuwa ukisema kuhusu**.Unaweza kuelezea zaidi?
Uliponiambia kuhusu**nilipata nikijiuliza kwa nini...
[Kwa kila jambo,** vinarejelea kile mzungumzaji anaelezea]
Huenda kukawa na hisia mbalimbali namatukio ya kihistoria hivyo kutatiza kuelewa kinachoendelea-hata kwa wahusika-kwa hivyo mwasilishaji mwenye hekima atawasilisha hoja zake poleploe na kwa uangalifu

Ni muhimu kuuliza maswali ya kufafanua kwa upole na utulivu ili usionekane kana kwamba unapingana.Hii ni mifano ya maswali kama hayo:

- Kuliendaje?
- Watu walisikia vipi hayo yalipofanyika?

Mifano ifuatayo ni ya maswali yasiyosaidia kwa sababu hayaruhusu majadiliano ama huwashurutisha watu kutoa jibu linalotarajiwa.

- Watoto wako wanaugua kila wakati?
- Una matatizo mengi katika jamii yako, sivyo?

Pia ni muhimu kuuliza maswali yanoyofafanua jukumu la imani

Kwa mfano:

- Watu wamewezaje kukabiliana na changamoto hizo?
- Kanisa linashughulikaje na jambo hili?

**Zingatia:** Ni muhimu wakati huu mwasilishaji kuhakikisha sauti za wanyavu, wadogo ou waoga, au wageni katika kundi wamesikilizwa (Taz.Mathayo 11:25).Huenda wakawa na maoni ya kuchangia katika hatua zote za mpangilio wa UWK na hasa maamuzi yanapofanywa.

## 2.3 Matembezi ya nyumbani na jamii

Njia bora ya kujenga uhusiano ni kuwaendea watu-si kungoja wao wakujie! Haya yanahusisha sehemu zote za Jeshi La Wokovu-Vikao, Vituo na makao makuu.Imependekezwa mbinu hii itumike mara kwa mara katika mpangilio wa UWK ili tujue zaidi juu ya jamii zetu, kuelewa matatizo yao, uwezo na changamoto zao.

Kuanzia siku za mwanzoni, Jeshi La Wokovu wameelewa umuhimu wa kuwa mitaani na kutembelea watu nyumbani.

Mbinu za usikilizaji na ufafanuzi zikisha elezwa imependekezwa watu watembelee sehemu hiyo pamoja na watu wa jamii hiyo.Katika matembezi haya wewe na mwanajamii muwe waangalifu ili kufaidika kutokana na mambo yanayowazingira na kisha kuyazungumzia.

Maombi ya kimya kimya husaidia wakati wa matembezi Ikiwa umealikwa, tembelea watu nyumbani kwao.

Kundi linahitaji kuuliza maswali ya ufafanuzi linapokutana na watu.Ujumbe unaotokana na shughuli hii unaweza kufuatiwa na majadiliano au kutambua mipaka ya sehemu zinazotembelewa.

## 2.4 Kuweka mipaka ya jamii

Mbinu ya kuweka mipaka ni njia nzuri ya kufanya watu kujua jamii na kuwafanya wanajamii kuthamini kile walichonacho.Kundi la watu lichukuwe jukumu la kutambua mipaka huku wakihakikisha mawazo ya watu tofauti na maoni yao yamejumuishwa.
Watu katika jamii wanaulizwa kuchora mchoro wa sehemu fulani.Ramani inaweza kutumiwa kuhimiza watu kuzungumzia jamii zao, rasli mali, mambo na matatizo yao.Utahitaji:

Mpangaji Ratiba-ana jukumu la kushughulikia karatasi,kalamu n.k,akihakikisha kila mtu katika kundi yupo na kila mmoja wao anaelewa jukumu lake

Zingatia: Jukumu lake ni kuandikisha umri, majina na historia ya wanakikundi na mambo muhimu yanayojitokeza na kubadilisha michoro kutoka chini mpaka kwa karatasi.

Mwasilishaji-Ana jukumu la kuwatambulisha wanakundi, kufafanua kazi inayotakiwa bila kuwapa matarajio makubwa.Anaongoza hatua ya kuweka mipaka akitumia maswali ya uwazi kuhakikisha kundi linahusisha wanajamii katika mpango huo.Anahakikisha hakuna anayetawala hali ya uwekaji mipaka, na hatimaye, anamaliza shughuli na kushukuru kundi kwa mchango wao.

Naibu Mwasilishi – husaidia mwasilishiaji kwa mipango ya uwekaji mipaka na kipindi cha maswali. Kwa mfano: “ni jambo gani ungependa libadilishwe katika jamii yako mnamo miaka 5 hadi 10 ijayo”? na hutumia maswali ya kindani kuyapekuwa zaidi mambo husika.

Wachunguzi – wana jukumu la kuonelea vile mwasilishi anavyotumia mbinu za uwekaji mipaka kwenye (mahojiano, maswala na kadhalika), kujumuishwa kwa wanajamii na hata ishara za mwili.Wachunguzi pia wanatakikana kuyatambuwa mambo yanayoenda sawa na yale yasio enda

**Zingatia:** Wanachama wa Jeshi La Wokovu katika Latin Amerika wameona umuhimu wa kuzingatia maswali matatu yafuatayo unapozungumza na watu katika jamii:

1. Je, matumaini na ndoto zako ni gani?
2. Mambo magumu ni yapi?
3. Jamii huyaonaje haya mambo/matunaini? Je wengine pia huyapitia?

sawa kwenye zoezi hilo na wawe waangalifu wa saa.

Baada ya kukamilisha zoezi la uwekaji mipaka, ni muhimu kuyapitia na kutafakari mafunzo yaliyopatikana

Maswali yafuatayo huenda yakawa muhimu:

- Ni mafunzo gani mapya yamepatikana?
- Ni yapi tuliyo jifunza mmoja kwa mwingine?
- Ni yapi yaliyoenda taratibu na kwa nini?
- Ni yapi hayakuenda taratibu na kwa nini?
- Majadiliano yalianziswa vipi? Unajuaje kama mambo yalienda taratibu?
- Mchoro ulianzishwa na nani? Kwa nini? Na ni nini kilitendeka badaye?
- Je wahusika walionekana kuvutiwa na huu mpango wa kuchora ramani? Je ulijuaje?
- Je mwasilishi aliwahi kulegea? Wakati gani? Kwa muda gani? Ni nini kilichotendeka kwa wakati huu?
- Kutoka kwa lile kundi ni nani aliyehusika sana na ni yupi hakujihusisha sana? Kwa nini?.
- Ni mbinu gani za usikilizaji zilitumiwa na mwasilishi? Je zilikuwa na usaidizi wowote?
- Mwasilishi alitumia mbinu gani za maswali? Ilikuwa na usaidizi wowote?
- Je michoro ilikuwa ya manufaa yoyote kwa majadiliano yenu? Kivipi?
- Je, ni jambo gani tunaweza kufanya vyema zaidi wakati mwingine?








## 2.5 Kujadiliana

Majadiliano hutumia mara nyingi mpangilio wa UWK unapotumiwa,hasa katika hatua ya 2 (Chunguza/Eleza) na Hatua ya 4 (Amua/Panga) Mbinu ya majadiliano ni rahisi na inaweza kutumiwa na yeyote mahali popote bila ugumu.Ili kuitumia unahitaji:

- Ubao,ubao mweupe au karatasi za kuandikia,au karatasi kubwa zaidi,
- mtu wa kuandika au kuchora ili kuonyesha vipengele tofauti;
- Mwasilishaji.

Kwanza kabisa jambo mada ni lazima itambuliwe (Hatua ya 1).Kisha katika Hatua ya 2 mwasilishaji anauliza kila mtu kuzungumzia chochote, mambo yaliyopita, mila, taswira, hisia au mambo megine yanayohusiana nayo.Mambo haya yote si mabaya katika hatua hii.Mwandishi anayaandika haraka iwezekanavyo, huku mwasilishaji akiwahiza watu kuendelea kutoa maoni.Unaweza kutoa muda wa kufanya haya, au uendelee hadi kila mtu atosheke kuwa wamesema kila walichokuwa nacho.

Kama kawaida ya kazi zote za uwasilishaji, ni muhimu kuwahusisha watu wanyamavu waoga na vijana.Hata hivyo, usiwashurutishe kuongea.Vivyo hivyo, wale wanaozungumza sana au kurudia jambo lile lile wahimizwa kusikiliza na kuwaachia nafasi wengine kuongea.
Baada ya majadiliano, mwasilishaji atasaidia kundi kuamua wanachotaka kufanya na maoni yao yote, Kundi litahitaji kukubaliana kuhusu malengo na madhumuni. Baadhi ya mbinu hizi zinaweza kusaidia katika hii hatua (kama vile 2.8 Kipau mbele)

## 2.6 Kutambua Uwezo na Vifaa/Mbinu

Mbinu hii husaidia sana katika Hatua ya 4 ya mpangilio wa UWK (Amua/Panga.)Ni jambo moja kwa kundi au jamii kuamua wanachotaka kufanya au mradi wanaotaka kutekeleza, lakini pia jambo tofauti kuaangalia kama wana vifaa na uwezo wa kutekeleza mradi huo.

Mwanzo wa Uwasilishaji wa Kiimani ni kutambua wingi wa mali, vipawa na mali wolizo nazo watu, familia zao, marafiki na jamii zao.Kila mtu-tajiri au masikini-wana vipawa vya kipekee na uwezo unaohitaji kutambuliwa na kukubaliwa.
Ingawa kila mtu,familia na jamii huwa na mali ya kuchangia,huenda wasiwe na yakutosha.Mbinu hii husaidia kutambua uwezo na mali iliyopo vile vile kutambua mapengo yanayohitaji kuzibwa kwa usaidizi kutoka nje ya jamii

Njia bora ya kufanya haya ni kugawa kundi mara mbili.
-Uliza kikundi cha A kujadiliana kuhusu vifaa na uwezo unaopatikana katika jamii au walivyonavyo
-Uliza kikundi cha B kujadili vifaa na uwezo unaohitajika kutekeleza mambo hayo.

Kisha yalete makundi pamoja ili kulinganisha orodha hizo mbili kisha watambue pengo kati ya 'tulichonacho' na 'kinachotakikana'Hatimaye kila mmoja anaweza kutoa maoni yake kwa vipengele 'vinavyokosekana' kwenye orodha vinyopatikana au njia badala zinazoweza kutumiwa ili jukumu lililoko linaweza kutekelezwa.Kufikia hapa, huu mtindo wa CPMS unaweza kusaidia kutambua usaidizi kutoka nje

## 2.7 Matumizi ya Biblia kwa Uwasilishaji wa Kiimani

Kuna njia tofauti za kupata maarifa ya Biblia kulingana na uwasilishaji na kutafakari 'tunachofanya na sababu za kukifanya.'

a) Tafuta vifungu vya Biblia, taswira na hadithi zinazohusiana na jambo/shughuli ambayo imetambuliwa (Hatua ya 1 katika mpangilio wa UWK).Labda utahitaji Biblia ya maelekezo au vianzilishi kusaidia kupata vifungu hivyo.Njia hii inaweza kuchukua muda mwingi lakini mafunzo au mambo mageni yanaweza kugunduliwa pasipokutarajiwa.

b) Majadiliano.Husaidia sana kundi la watu wanapopata vifungu mbalimbali vya Biblia vinavyohusiana na jambo/shughuli.Kisha inafaa mchague moja halafu mkisome pamoja.Njia hii inaweza kusaidia watu kuona mambo kwa njia mpya kutokana na watu tofauti kutoa maelezo yao hivyo kuwafanya wengine kung'amua mambo mapya.Kundi lihimizwe kuchagua mafungu ya Biblia ambayo yanatatiza siyo yale wanayoyaelewa. Kumbuka Roho Mtakatifu wakati mwingine anakuwa 'msumbuaji' na pia 'mfariji'

c) Jifunze kutokana na mafungu yaliyochaguliwa.Wakati mwingine ugunduzi na kuelewa mambo mapya kuhusu hali hutokana na kuangalia tu kifungu fulani.Au unaposoma kitabu kimoja tu katika Biblia unaweza kuchukua sura ya hiyo siku na uone ikiwa kuna ukweli unaolingana na hali hiyo.Ama unaweza kutumia kifungu hicho 'ulichopewa 'kupitia kwa mahubiri au mafundisho ya Biblia kanisani.Umakini na uaminifu katika kujibu maswali yanayojitokeza kutokana na kifungu cha Biblia,ni muhimu kwa kuzingatia shughuli hii.

d) Vifungu vya Biblia vya kukuongoza katika uwasilishaji.Tafadhali usijifunge tu kwa vifungu na mistari iliyotolewa unapofanya masomo ya Biblia:Hata hivyo,vifungu vifuatavyo vinaweza kusaidia:

Kumbukumbu La Torati 10:12-20; Kumpenda Mungu kunajumuisha kuwapenda wajane,mayatima na wageni
Ruthu;Soma kitabu kizima
1 Samueli 16:7;Mungu huangalia moyo
2 Smueli 12:1-13; Daudi kutumia mamlaka vibaya kujinufaisha,kisha kutambua na kukubali makosa yake
I Yeremia 1:10;Vunjavunja kisha upande tena
Isaya 61:1-4 Habari njema kwa wanyanyaswao;ujengaji upya wa miji iliyoharibika na vizazi vingi vilivyoangamizwa
Ezekieli 37:1-11; Roho wa Mungu hupeana miili mipya, hupumua maisha mapya kwa kile kilichokuwa tu bonde la mifupa iliyokauka
Hosea 1-3;Uaminifu wa Hosea kwa mke wake licha ya kuwa kahaba unalinganishwa na upendo wa Mungu wa kudumu kwa watu wake,hata kama



wamemmuacha na kumuasi
Mathayo 4:1-11;Majaribio ya Yesu jangwani
Marko 6:39-44 na Luka 9:10-17;Linganisha hadithi hizi mbili kuhusu ulishaji wa watu elfu tano
Luka 5:12-16; Yesu anaponya mtu aliyeathiriwa na ukoma
Luka 8:42-48; uponyaji wa mwanamke 'mchafu' aliyetokwa na damu
Luka 15:1-7;Upendo wa Mungu kwa waliopotea na kukataliwa
Luka 18:9-14; Mfarisayo na mwenye dhambi
Yohanh 4:1-26;Mwanamke Msamaria katika kisima
Yohana 8:1-11;Mwanamke alipatikana akizini
Yohana 9:1-5; Yesu aponya mwanamme aliyezaliwa kipofu (ugonjwa au dhambi?)
Wakolosai 3:3; Maisha yaliyofichwa kwa ndani ya Kristo na Mungu
1 Timotheo 3:1-13;Sifa za viongozi
Yakobo 2:1-13; Maana hasa ya kumpenda jirani yako
1Petero 3:4; Roho pole na nyenyekevu
1 Petero 4:13;Kushiriki katika mateso ya Kristo

## 2.8 Kuyapa mambo kipau mbele

Mbinu hii husaidia kukiwa na mambo mengi ya kushughulikiwa katika (Hatua 1).Pia husaidia katika Hatua ya 4 (Amua/Panga) kusaidia kuchagua mapendekezo ya kutekelezwa kutoka kwa maoni mbalimbali.

Baada ya kutambua mabadiliko au mageuzi tofauti yanayohitaji kufanywa,kundi au wawakilishi wa jamii watahitaji kuamua,wakitumia maarifa yaliyopo, maoni yapi yakutekelezwa kufuata mpangilio upi.Baada ya majadiliano,huenda kukawa na takriban maoni 30 lakini kundi litatakiwa kuamua tatu au nne mwanzoni.Njia rahisi lakini nzuri ya kusaidia kundi kukubali mambo ya kupewa kupau-mbele ni:

- Maoni yanaorodheshwa kwa umakini, kila likisimamiwa na neno kifungu au picha.
- Mwasilishaji anahakikisha kila mtu anaelewa kila kiwakilishi
- Neno hilo, kifungu au picha ya kila pendekezo linaandikwa au kuchorwa katika karatasi tofauti.Hivi viwakilishi vinawekwa mahali tofauti katika nafasi iliyopo.
- Kil mtu anapewa idadi sawa ya vijiwe, maharagwe na vihesabu.
- Kila mtu anaweka idadi fulani ya vijiwe n.k kwa kila pendekezo, kuonyesha umuhimu ambao wangekipa.Kwa mfano, kama ni muhimu sana kwao, wanaweza kuweka chini vijiwe 5.Wakiona si muhimu wanaweza kuweka kijiwe kimoja au wasiweke chochote.
- Baada ya kila mtu kumaliza, vijiwe n.k vinahesabiwa.Pendekezo likiwa na vijiwe vingi, kundi linachukulia kuwa ndio pendekezo muhimu.
- Halafu matokeo yanajadiliwa kwa usaidizi wa mwasilishaji.

## 2.9 Kufikiri kwa Ubunifu

Mbinu hii hutumika sana katika Hatua ya 3-Tafakari/Chunguza.Pia inaweza kutumika katika hatua yoyote ya jambo linapofanyika kunapokuwa na matatizo au mambo yanapokwama.Watu huwaza kwa njia tofauti.Kwa watu wengne kuwaza kwa ubunifu hufanyika kwa urahisi kuliko kuwaza kwa maneno na kila mtu hufaidika kutokana na kujaribu mitazamo ya kuwaza kwa ubunifu mara kwa mara.Jambo hili ni kweli kabisa unapotafakari na kuwa na fikira pana na msikivu kama ilivyo katika Hatua ya 3 kwa mpangilio wa UWK.

Kuhimiza watu kutenda maoni yao kwa hali fulani ama mapendekezo au kuimba na kuigiza pamoja ili kuelezea hisia zao, husaidia katika wakati tofauti wa uwasilishaji.Mambo haya huchangamsha washiriki na kuwapa muda wa kupumzika. Baada ya muda huo wa kufikiri kwa ubunifu,na labda wakati wa maombi na kushirikiana,mawazo mapya na fikira zinaweza kuibuka.Hasa uhusiano kati ya mafundisho na mafunzo kutoka kwa Biblia yanaweza kutokea na kuchangia pakubwa katika hatua ya kutathmini na kutafakari

## 2.10 Mbinu ya Kutatua Matatizo

Mbinu hii inaweza kutumika katika hatua yoyote ikiwa watu wanaacha kushirikiana au wakiwa na fikira tofauti .Kufuatilia hatua za UWK na mwasilishaji mzuri, hupendeza na hustahili. Hata hivyo,washiriki



wakichoka au mambo kushindikana,huona ugumu kuendelea na hatua ya kutathmini na kutafakari na hivyo kukosa subira ya utekeleza. Katika hatua zingine watu wanaweza kukosa umakini hivyo kuanza kufikiria mambo mengine.Haya yakitokea,itakuwa bora mwasilishaji ku: Tafuta shida iko wapi na kinachosababisha shida hiyo(kuangazia shida pasipo kumlaumu yeyote) Uliza watu sababu za kufikiri kuwa kuna shida. (Kuzungumzia shida pasipo kulaumu).

Waulize washiriki wanaotofautiana kabisa kimawazo kubadilishana viti au wanapoketi kisha waseme maoni ya mwenzao au imani yoa kwa ukweli kabisa.Haya yatawasidia ‘kuvaa kiatu cha mwenzake’.Baada ya haya, uliza maoni kuhusu hisia za wanaoshiriki.



UPENDO
KUJIPIMA
5
4
3
2
1
Afyia
IGAs
(Merry go round)
HBC
KWINA
THE SALVATION ARMY

Pendekeza wakati wa mapumziko na kutumia muda fulani kwa kisa cha ubunifu pamoja kabla ya kuendelea na kipindi. Waalike wapendekeze masharti ya kufuatwa ili kusaidia kukamilisha jukumu lao.

Jadili makubaliano ya kuandika Ratiba itakayofuatwa ili kukamilisha jukumu hilo

**Zingatia:** Kama mdhamini kutoka nje amehusishwa, mbinu zingine za kutathmini zinaweza kutumika.Hata hivyo mbinu ya kujitathmini pia inafaa kutumiwa kwa maana itahusisha kila mtu katika kundi na vile kazi yao inavyoendelea.Haya yatawasaidia kuwajibika na kutia nguvu zaidi katika kazi hiyo..

### 2.11 Mbinu ya Kujitathmini

Kujitathamni husaidia kundi kujua kama wanafanikiwa kufikia malengo na dhamira yao.Mbinu hii imesaidia makundi mbalimbali ya Jeshi La Wokovu.

Wakati wa mkutano wa makundi tumia mbinu ya ,majadiliano( 2.5) kukubaliana malengo na dhamira itakayotathminiwa.Kwa mfano,lingekuwa kundi la vijana linalotathminiwa,wanaweza kuhusisha mambo kama,idadi ya watu wanaohudhuria;shughuli mbalimbali,ubora wa chakula kilichoko;muda wa maombi;idadi ya wageni walioalikwa;idadi ya watu wanaojadili mambo na kiongozi.
Tumia karatasi kubwa na uchoro mistari miwili ya grafu (yaani mstari wa X na Y) Katika mstari wa Y (wima) andika nambari 0, 1, 2,3,4,5 kwa mtindo wa kuongezeka.Wacha mstari wa X (unaopita kati) bila nambari yoyote hadi wakati wa mkutano wa kundi.Baada ya kuafikiana mambo ya kutathmini, kundi sasa lijadiliane kiwango cha kutuza kila jambo, kuanzia kwa 0=vibaya zaidi hadi 5=vizuri zaidi.Baada ya kutuza.Watu katika kundi wachore matokeo kwa grafu, kisha wanaweza kujadili njia za kuinua kiwango hasa kupunguza udhaifu.

## Maswali Yanayoulizwa Kila Wakati

1. Uwasilishaji Wa Kiimani ni nini? Uwasilishaji Wa Kiimani (UWK) ni mpangilio na mbinu kadhaa zinazosaidia watu kufikiri, kuzungumza, kafafanua na kushughulikia maswala yao wakitumia imani.Hatimaye hupata watu na jamii zilizokomaa.UWK hutumia mpangilio wa kutafakari mambo ya kidini ukiboreshwa na mbinu za sayansi jamii

2. Kwa nini Jeshi La Wokovu hutumia Uwasilishaji wa Kiimani?
Jeshi La Wokovu wanaamini kuwa imani ni kipengele muhimu katika kuimarika kwa watu na jamii zenye afya.Imani haitilii mipaka uwezo wa Jeshi La Wokovu kama ilivyoelezwa kwenye madhumuni yake, 'kusaidia watu kupata mahitaji yao bila ubaguzi'; ila Imani katika Mungu Baba, Mwana na Roho, ndio msingi wa kazi zote za Jeshi La Wokovu.Hata hivyo, mambo yanayohusiana na imani yanafaa kuchukuliwa kwa hekima



na uangalifu hasa katika jamii ambazo zina watu wa imani tofauti tofauti. UWK hupendekeza mpangilio na mbinu mbalimbali za kusaidia katika hali kama hii.Mtazamo huu ni sambamba na mafundisho ya msingi ya Jeshi La Wokovu pamoja na mafunzo ya dini,Maagano na Sheria na Kumbukumbu Rasmi za mikutano

**3. Je, Uwasilishaji Wa Kiimani ni wa waumini wa Jeshi La Wokovu pekee?** La, unaweza kutumiwa na watu wengi.Jeshi La Wokovu wanaamini injili ya Kikristo inaweza kubadilisha kila sehemu ya maisha (mwili, fikira na roho) na inaweza kufaidi kila mtu, kila mahali.Jukumu la Jeshi La Wokovu ni kuwapa watu injili yote kwa mtu mzima na ulimwengu wote.

Uwasilishaji Wa Kiimani husaidia mabailiko haya kutokea.Matumizi ya mpangilio wa UWK na mbinu zinaweza hutoa nafasi kwa watu wa imani tofauti na mitazamo wa kimataifa kufanya kazi pamoja.Matokeo yake ni mahusiano mwafaka, watu wenye afya nzuri na jamii zenye uwezo mkubwa.

**4. Uwasilishaji Wa Kiimani unaweza kutumiwa vipi?** Huu si 'mradi' wala 'kipindi' lakini ni njia ya utendaji kazi katika Jeshi La Wokovu.Inaweza kutumika katika sehemu zote za Jeshi La Wokovu, pamoja na maendeleo ya jamii, kazi ya jamii.afya, huduma za dharura, mahubiri, maamuzi ya uongozi, ushauri n.k.Mpangilio na mbinu za UWK husaidia wakati wa kutunza, kujifunza, kupanga na kufafanua maswala.

**5. Ni nani anayeweza kutumia Uwasilishaji Wa Kiimani?**

-Watu binafsi wanaweza kutumia mpangilio wa UWK na mbinu zake kutatua matatizo yao kivyao (ingawa mbinu nyingi hutumika vizuri katika makundi)

-Kundi linalofanya kazi pamoja katika jamii linaweza kutumia UWK katika shughuli zao za kila siku hasa, katika utunzaji, usomaji, utatuzi na utetezi wa maswali mbali mbali.



-Kundi la kutoka nje-kundi la watu linaweza kuungana na jamii kujenga uhusiano kwa kutumia Uwasilishaji Wa Kiimani kuhimizana na kupata masomo.

**6. Uwasilishaji Wa Kiimani umejengwa kwa mambo gani ya kimsingi?** Mambo matano yametambuliwa kama msingi wa mtazamo wa watu kupitia kwa UWK:

Jamii-Jeshi La Wokovu wanaamini kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu.Uwasilishaji Wa Kiimani kusaidia kujenga uhusiano mwafaka na watu wote-hasa masikini na wale waliotengwa katika jamii zetu. Kubadilisha watu na jamii ni mwito wa wakristo wote na UWK husaidia watu kushirikiana vizuri na Mungu kutimiza huduma yake ulimwenguni. Neema-Mungu hapatikani tu mahali patakatifu kama makanisa au

hekalu.Watu wa imani wanatakiwa kuwafikia watu wa jamii zao, wakijenga uhusiano na watu wengi iwezekanavyo kwa sababu neema ya Mungu ni ya kila mtu na inapatikana kila mahali.

Tumaini-Wawasilishaji wa Kiimani wanaamini katika uwezekano wa mabadiliko yanayoleta maisha bora sasa kama tumaini la maisha ya milele Kujali-Wawasilishaji wa Kiimani hutafuta kusaidia watu wakati wote.Matokeo yake ni kule kutaka kuwapa watu usaidizi katika wakati mgumu na wa shida bila kuwatumia kukidhi haja zao.

Mabadiliko-Wawasilishaji Wa Kiimani wanaamini kila mtu anastahili kuishi maisha ya maana.Kwa hivyo mabaliko katika uchumi,mazingira na elimu yanafaa kupimwa na kufuatiliwa.Matokeo muhimu ya UWK ni uboreshaji wa kiroho na kiafya.Mtume Paulo alitaja sifa za watu wanaomcha Mungu na wenye afya nzuri:' upendo, amani, uvumilivu, huruma, ukarimu, uaminifu, upole kiasi' (Wagalatia 5:22-23)

Uwasilishaji Wa Kiimani unachukua muda upi kukamilika? Muda unategemea majukumu yaliyoko.Wawasilishaji wazoefu hujua wakati wa kuendelea na hatua inayofuatia lakini mara nyingi watu huhitaji muda wa kutosha kushughulikia hatua nne ambazo zitakuelekeza kwa hatua ya tano-utekelezaji.Hilo ni jambo nzuri-uhusiano huchukuwa muda kuimarika na watu wanahitaji muda wa kutosha kuelewa ujumbe unaotokana na mpangilio wa UWK.Usiharakishe!

8 Je, hili ni jambo geni? La.katika historia ya mwanadamu,watu wenye imani wamekuwa na njia za kuhusisha imani yao na matendo.Jeshi La Wokovu wamechukulia msimamo huu kwa umakini.UWK hufuata msingi wa kazi ya miaka michache iliyopita ya Jeshi La Wokovu kama vile kueneza injili na wengine.Mbinu za kukuza jamii,ushauri wa jamii,uongozi wa kiutumwa.SALT,kushauriana kupitia hisia za Kijamii n.k.Mpango wa UWK huchangia na kukuza mafundisho mengine.UWK hutumia mipangilio mahsusi na mbinu zinazohitaji kufunzwa ili ziwe za kutumiwa kila wakati.Huu ni mtazamo mpya kwa watu wengi.

9. UWK unaingiliana vipi na mtindo wa CPMS? CPMS ni mtindo unaotumia mbinu za Jeshi La Wokovu kuongoza na kusaidia miradi ya jamii inayopata usaidizi wa kimataifa.UWK ni njia inayotumiwa na Jeshi La Wokovu katika sehemu zote za huduma.Mara nyingi katika Hatua ya nne ya mpangilio wa UWK,kunaweza kutokea pengo la msaada fulani unaohusiana na jambo muhimu katika jamii.Katika hali hii,mtindo wa CPMS unaweza kutumiwa kapata msaada kutoka nje ambapo jamii itaweza kufikia malengo yao.Maarifa na ujuzi unaopatikana kutokana na mpangilio wa UWK unatakiwa kutumiwa kutayarisha mtindo wa CPMS unaotoa mwongozo wa mapendekezo ya miradi.

10. Ninaweza kupata wapi maelezo zaidi? Uchunguzi wa mambo mbalimbali na mbinu zinaendelea kutayarisha vifaa. Vifaa na mbinu zilizoidhinishwa na Makao Makuu ya Idara ya Kutayarisha Vifaa vya Vipindi vinapatikana

www.salvationarmy.org/fbf



### MWASILISHAJI MZURI WA KIIMANI

- Anathamini kila mtu
- Huzikiliza kwa makini
- Huhimiza watu kushiriki
- Amejiandaa vizuri
- Huthamini maoni ya wengine
- Ni mvumilivu
- Ni mwepesi
- Amepevuka
- Huhimiza wengine
- Hutumia mbinu na mitazamo mbali mbali
- Huendeleza jambo bila kushurutisha matokeo
- Hukubali makosa na kujifunza kutokana nayo
- Anasikiliza kazi ya Kairos
- Anahimiza watu kusoma zaidi hadithi za Biblia

### MWASILISHAJI WA KIIMANI ALIYE NA UPUNGUFU

- Anapenda kuthihibiti
- Analazimisha watu kutoa majibu
- Ana haraka
- Anahukumu
- Hajali
- Anaongea sana
- Analazimika maoni yake kwa wengine
- Anajigamba kujua mengi
- Hatikisiki
- Anawapendelea wanaozungumza sana
- Anawapuuza wanyamavu
- Anafuata ratiba bila kulegea
- Hana uhakika wa kutumbia mbinu za Uwasilishaji Wa Kiimani